Julai 2021

JE, MIKATABA YA BIASHARA HURU (FREE TRADE AGREEMENTS) INA MAANA GANI KWA WANAWAKE WA KIAFRICA?

Uchambuzi wa Kina Kuhusu Mkataba wa Biashara Huru Barani Afrika (African Continental Free Trade Area-AfCFTA)

Mfanyabiashara wa vyakula akiandaa vibanzi yaani chips kwa ajili ya wateja wake katika soko la Wandegeya la Kampala Uganda.

Seed Savers Network Kenya

THE SUHODE FOUNDATION

GRAIN

Eneo la biashara huria Barani Afrika (AfCFTA) lililo idhinishwa hivi karibuni linashamiri kote barani Afrika. Huu ni mpango wa umoja wa mataifa ya Afrika ulio na lengo la kuimarisha biashara miongoni mwa mataifa haya, kupanua na kuunganisha masoko katika kanda hii. Watetezi wa AfCFTA wanasema kuwa mpango huu utalibadilisha bara la Afrika na kulifanya kuwa lenye nguvu za kiuchumi. Lakini kwanza hebu tutilie mkazo kwenye kundi moja la idadi ya watu, kundi ambalo ni maarufu katika kilimo: makubaliano haya ya kibiashara yana maanisha nini kwa wanawake wa Kiafrika na jukumu lao katika uzalishaji wa chakula na kilimo-biashara barani Afrika?

Mikataba huru ya kibiashara sio mipya barani Afrika

AFCFTA inafuata malengo yale yale ya mikataba mingine ya kibiashara ambayo nchi za kiafrika zimehusika nayo katika miongo ya hivi karibuni, kwa sasa AfCFTA inayafunua malengo hayo kwa kiwango kipana zaidi. Malengo yote yanalenga kuimarisha mazingira ya kibiashara na ajenda ya wawekezaji ambayo zamani ilikuwa imewekwa katika kanda kadhaa za Afrika kupitia mikataba na michakato kadhaa ya uwekezaji.

Katika mwaka wa 2000, Marekani ili idhinisha na kuzindua sheria iitwayo Sheria ya Ukuaji na Fursa ya Afrika (*Kwa Kiingereza: Africa Growth and Opportunity Act - AGOA*) sheria ambayo ni ya upande mmoja inayolenga kuruhusu mataifa ya Kusini mwa Jangwa la Sahara kufikia masoko ya Marekani pasipo kutozwa ushuru. Uhuru huu kibiashara pasipo ushuru ulihusu zaidi ya bidhaa 6000 ikiwemo nguo, mavazi, viatu, vyakula, maua na bidhaa zingine. Hata hivyo, chini ya sheria hii kuna nchi baadhi za Kiafrika ndizo zilizochaguliwa kuwa zinastahili na kukidhi viegezo na masharti yaliyowekwa na Marekani.

Hata hivyo, miaka ishirini baada ya kuzinduliwa, mpango wa AGOA umekuwa na mafanikio machache mno. Ni nchi tatu tu za Kiafrika ambazo ni Angola, Afrika Kusini na Nigeria ndizo zilizo jumuishwa kikamilifu katika mpango huu. Mauzo ya nje kupitia mpango wa AGOA kutoka Afrika kwenda Marekani yamepungua badala ya kuongezeka, kutoka dola za kimarekani bilioni 68.2 mwaka 2011 hadi dola za kimarekani bilioni 23.2 mwaka 2014. Kama hiyo haitoshi, utawala wa Trump kwa sasa umehamia katika awamu mpya ya mikataba ya kibiashara na nchi za Kiafrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, na utawala huo umeanza na Kenya. Watalaamu wanasema kuwa makubaliano hayo kati ya Marekani na Kenya yatafuta mwelekeo usio wa haki na uliopingwa kati ya Marekani na Morocco.

Kama ilivyo kwa Ulaya, tangu enzi za uhuru, nchi za Afrika, Karibeani, na Pasifiki kwa pamoja zilijihusisha na Umoja wa Ulaya kupitia mipango ya makubaliano. Mpango wa kwanza ulikuwa ni Azimio la Yaounde lililofuatiwa na Mikataba ya Lome I-IV na Mkataba wa Ushirikiano wa Cotonou. Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, kumekuwepo na Mikataba ya Ushirikiano wa Kiuchumi *(Kwa Kiingereza: Economic Partnership Agreements - EPAs)* ambayo imekuwa na dosari kwa kufuata mfumo wa maeneo madogo madogo. Hata hivyo, ni makubaliano ya muda tu ndiyo yaliyokamilika hadi sasa na kati ya hiyo ni michache ndiyo inayofanya kazi.

Msichana kijana akichambua mboga za majani kibichi katika kaunti ndogo ya Gweri, Wilaya ya Soroti, Uganda. Picha: Nobert Petro Kalule.

Jumuiya ya Ulaya ya Biashara Huria (EFTA) – inayoziunganisha nchi za Uswizi, Norway, Iceland, na Lichtenstein pia imekuwa ikisukuma uwepo wa Makubaliano ya Soko Huria (*Kwa Kiingereza: Free Trade Agreements – FTAs)* na nchi za Kiafrika ambazo ni washirika wake. Mikataba hii ni ya kina sana kiasi kuwa baadhi ya mataifa ya Magharibi kama vile Marekani na yale ya Umoja wa Ulaya yanapendelea.

Kwa upande mwingine, Japani na Uchina hazijaingia mikataba yoyote ile ya kiabiashara na Afrika. Ila wao wamekuza makubaliano maalum ya uwekezaji na misaada kwa nchi moja moja binafsi za Afrika na pia kupitia maeneo na kambi ndogondogo za bara la Afrika.

Kihistoria, biashara rasmi ya ndani miongoni mwa mataifa ya Afrika yenyewe imekuwa ndogo katika miongo kadhaa iliyopita ikifikia asilimia 2 tu ya thamani ya jumla ya mauzo ya nje na uagizaji wa bidhaa toka nje. Na hali hii ndiyo inayolengwa kushughulikiwa na makubalino ya biashara huru ya Afrika (CFTA).

Wanawake na biashara barani Afrika: Athari zilizojitokeza hadi sasa

Ni muhimu kuzingatia kuwa sehemu kubwa ya biashara ndani ya Afrika, yaani ndani ya nchi za Afrika na hata mipakani ni biashara isiyo rasmi. Ni vigumu kupata takwimu lakini picha ya jumla inaonyesha kuwa inachangia asilimia 30 - 40 ya biashara ndani ya Afrika. Katika nchi kama vile Afrika Kusini, ambapo asilimia 40 ya watu wanafanya biashara isiyo rasmi, takribani asilimia 70 ya biashara hizo ni katika biashara ya chakula. Mwelekeo huo ni sawa katika bara lote: sehemu kubwa ya biashara hii inahusisha chakula na bidhaa nyingine za kilimo. Wanawake ndio kundi kubwa linalohusika, ambapo katika maeneo ya vijijini, wanawake wanachangia takribani asilimia 60 ya nguvu kazi katika kilimo na hadi asilimia 80 katika shughuli nzima ya uzalishaji wa chakula. (Angalia Sanduku 1: Wanawake katika Kilimo barani Afrika)

Sanduku 1: Wanawake katika kilimo barani Afrika

Matumizi ya wakati kwa wanawake katika kilimo hutofautiana kulingana zao husika, mzunguko wa uzalishaji, umri na aina ya vikundi vya kikabila, lakini kupalilia na kuvuna kwa ujumla ni majukumu ya wanawake na pia hujumuisha sehemu kubwa yamajukumu ya kaya yasiyokuwa na malipo kama vile kuandaa chakula, kutafuta na kukusanya kuni, na pia kuchota maji. Ushiriki wao katika kazi za masoko vijijini hutofautiana

katika maeneo yote, lakini mara kwa mara, wanawake ndio bado hawalipwi, mara nyingi huwa ni wafanyakazi wa msimu ambao hulipwa malipo kidogo kuliko wanaume kwa kiwango sawa cha kazi. Uwepo wao unatambuliwa haswa katika sekta ya ukuzaji matunda, mbogamboga na maua yanayouzwa nje ya nchi.

Shughuli zao katika sekta hii ni pamoja na uzalishaji wa mazao ya kilimo, kuchunga wanyama, kusindika na kuandaa chakula, kufanya kazi kwa mshahara katika biashara za kilimo na biashara zingine vijijini, kutafuta kuni na kuchota maji, kushiriki katika biashara na uuzaji, kuzitunza familia na nyumba zao. Pamoja na majukumu hayo, wanawake wanatambulika kwa jukumu lao kubwa katika uhifadhi wa mbegu barani Afrika. Wanawake wanatambulika kuwa wao ndio watunzaji wakuu wa mbegu kwa kuwa wanafahamu namna ya kuzichagua na kuhifadhi mbegu mbalimbali na kuweka akiba kwa siku zijazo, na jukumu hili linaonekana katika jamii nyingi za Kiafrika. Shughuli hizi nyingi hazitambuliki kama "ajira hai kiuchumi" katika taarifa nyingi za kitaifa lakini shughuli hizo ni muhimu sana kwa ustawi wa kaya za vijijini.

Taarifa za zamani za mikataba ya biashara huria inadhihirisha kuwa haiboreshi nafasi ya wanawake na wala haishughulikii matatizo ya wanawake yaliyoelezwa hapo awali katika jamii na isitoshe hakujawa na faida nzuri kutokana na mikataba hiyo kwa wanawake. Wadadisi wanaotetea haki za wanawake wanapinga mikataba ya kibiashara huria kwa Afrika kwa kuwa hutumia upungufu uliobainika na unaoweza kukandamiza haki za wanawake katika maeneo yao. Mambo muhimu yaliyojitokeza ni:

- Kimsingi, mikataba ya biashara huria inahusianishwa kwa karibu na mapambano ya haki za wanawake kwa sababu inachangia na kuendeleza **unyonyaji kwa kutoa ajira duni** ili kupata utajiri wa kusafirisha nje. Hii ni kwa sababu wanawake ndio wanaounda hilo kundi kubwa la wafanyakazi, yaani wale wanaolipwa na wasiolipwa. Tangu mkataba wa biashara huria wa Amerika ya Kaskazini uliposainiwa kati ya Marekani, Canada na Mexico mwaka 1993, ikifuatiwa na kuanzishwa kwa Shirika la Biashara Duniani (World Trade Organization) mwaka 1995, mikataba ya biashara na uwekezaji imetumika kwa kuendeleza mtindo wa kiuchumi unaowafaidisha wachache na kuleta hali isiyo ya usawa kinjisia, tabaka na rangi duniani.
- **Ubinafsishaji wa mbegu** kupitia sheria za umiliki, unadhoofisha uwezo wa wanawake kupata mbegu za kupanda na kuwanyima haki ya kuhifadhi mbegu, kubadilishana mbegu na kufanya majaribio ya mbegu mambo ambayo yanaunda nguzo muhimu katika kilimo endelevu. Katika Afrika, nchi kama Algeria, Morocco, Misri, Tunisia, na Afrika Kusini tayari wameshafungwa mikono kwa kukubali kufuata viwango na taratibu za UPOV ndani ya mikataba ya kibiashara na Marekani (US), Umoja wa Ulaya (EU) na nchi wanachama wa EFTA. UPOV inazuia sana haki hizo za kuhifadhi mbegu na inafungua mlango wa hakimiliki kamili ya mbegu ambazo zimefanyiwa mabadiliko ya vinasaba (transgenic) hapo baadaye. Na bado wanawake ni kiini cha kazi ya kuokoa mbegu barani Afrika. Ikiwa wanawake hawataweza kuendelea kuchukua jukumu lao katika kuokoa mbegu, na ikiwa hatawasimamia jukumu la ya kiuchumi katika jamii, na ikiwa hatawatajiinua katika michakato ya kufanya maamuzi, basi ni hakika kuwa hatimaye nguvu zao kama wanawake zitakuwa zimedhoofishwa na kumomonyoka.
- **Upatikanaji wa dawa** ni suala jingine lenye kuleta wasiwasi kwa wanawake ambao mara nyingi hupata changamoto zitokanazo na sheria za haki ya umiliki zitokanazo na mikataba ya kibiashara. Kwa mfano, Afrika ya Kusini imechangia pakubwa katika vita ya kulegeza haki za umiliki wa madawa katika mikataba ya FTA na WTO barani Afrika. Hili ni muhimu katika kuhakikisha sekta hii inakuwa na usawa na uhuru hasa katika wakati huu tunapokabiliwa magonjwa ya mlipuko kama vile COVID-19.
- **Ubinafsishaji wa maji**, unaotokana na uhuru wa utoaji wa huduma, mara nyingi umesababisha kupunguza upatikanaji wa maji, haswa kwa jamii masikini na huongeza mzigo kwa wanawake ambao hulazimika kuamka mapema na kwenda mbali kutafuta maji kwa ajili ya kaya zao. Katika Afrika nchi kama Tanzania, Ghana na Afrika Kusini wameshuhudia matatizo haya kutokana muktadha wa sera za ukopeshaji za Benki ya Dunia (World Bank) na Shirika la Fedha Duniani (IMF). Mataifa ya Ulaya yanaweza kuanza kutetea haki pana za wawekezaji na wanaweza kuleta hoja kuhusu upendeleo maalum kwa makampuni yao ya maji hasa katika wimbi lijalo la mazungumzo ya EPA na mataifa ya Kiafrika.
- **Kanda maalum za kiuchumi** ambazo biashara huria na mikataba ya uwekezaji huendeleza na kuwa na vifungu vinavyochochea unyonyaji wa wanafanyakazi wakiwemo wanawake. Kwa kuwa kanda hizi zinafanya kazi mbali na mazingira ya sheria ya wafanyakazi na

zile za kimazingira, mara nyingi huwa zina mazingira mabaya kabisa kwa wafanyakazi: kama vile malipo duni, makazi duni, na kiwango cha chini cha usafi, vitu ambavyo kwa ujumla wake huzaa utamaduni wa unyanyasaji dhidi ya wanawake. Idadi kubwa ya nchi barani Afrika zina kanda maalum za kiuchumi, maeneo ya viwanda na uwekezaji ambapo maswala ya ardhi na kanuni zingine za biashara zimelegezwa na tayari zina madhara mazito kwa wanawake. Kwa hivyo itakuwa kero kuona zimehalalishwa na kukita mizizi zaidi kupitia kizazi kijacho cha FTA ikiwemo mkataba wa Biashara Huria Barani Afrika (AfCFTA).

- **Kampuni za upandaji miti kilimo-biashara**, ambazo zinachochewa na kulindwa na sheria za uhuru wa uwekezaji wa mikataba ya biashara, huondoa wakulima wadogo kupitia unyakuaji wa ardhi na kisha kuhamasisha na kukuza mfumo wa chakula cha viwandani ambao si endelevu. Makampuni makubwa ya chakula kama Nestle na Danone yamewekeza sana barani Afrika katika sekta ya maziwa, kahawa na katika bidhaa zingine za chakula wakilenga masoko ya ndani na nje ya bara hili. Makampuni makubwa ya maduka ya Kiafrika kama Naivas nchini Kenya ama Shoprite kutoka Afrika Kusini huvutia ufadhili kutoka mataifa ya Magharibi na kuwagawia faida kubwa kutokana na mapato yao. Maduka makubwa kutoka nchi za Magharibi yakiwemo Carrefour na Auchan wamewekeza barani Afrika na kusababisha ushindani mkali katika masoko ya ndani. Makampuni ya dawa na mbolea za kilimo kama Yara, Syngenta na Bayer hulenga kupata fedha zaidi kutoka kwa wakulima wa bara la Afrika licha ya athari mbaya ya pembejeo hizo katika ardhi, bioanuwai na rasilimali za maji ambazo wanawake hutegemea kukidhi mahitaji yao.

Shinikizo hili la kupanua mtindo wa kilimo cha mashamba makubwa, mtindo ambao umekuwa ukiendelezwa Afrika tangu enzi za ukoloni ulielemea vibaya maslahi ya wanawake. Kilimo cha upandaji miti na mashamba mengine makubwa huahidi ajira lakini kwa kawaida huwa ni ajira zenye malipo duni na huwanyima wanawake uhuru wakunufaika kutokana na misitu, maji safi, na huduma za afya zinazo jitosheleza, na mara nyingi ni uwekezaji unaochangia sehemu kubwa ya ukatili dhidi ya wanawake.

Hali hii inaongoza na kuwa ya kushangaza hasa tunapokabiliana nayo leo: katikati ya maafa ya janga la COVID-19, wakati ambapo Shirika la Chakula Duniani (World Food Programme) limeonya juu ya uwezekano wa baa la njaa "yenye uwiano na maelezo ya Biblia" katika nchi kumi, na kati ya nchi hizo nusu yao zipo barani Afrika, ni ajabu kuona Afrika ya Mashariki inasherehekea chakula chao kupelekwa huko Brussels chakula kinachotoka katika tasnia ya kilimo-bustani hasa maua, mboga, na matunza kilimo kinachoendeshwa na viwanda vya Ulaya.

Tukitamatisha, ni vyema tutambue na kuelewa uhusiano uliopo kati ya makubaliano ya biashara huria na uwekezaji, wanawake na uendeshaji wa kijeshi barani Afrika. Je, ni bahati mbaya kuwa serikali ya Trump inatoa Mkataba wake wa Biashara Huru barani Afrika (FTA) kwa Kenya, ambaye ni mshirika muhimu wa serikali ya Marekani katika kupambana na ugaidi katika eneo hilo?

Je Mkataba huu wa Biashara huru utakuwa tofauti?

AfCFTA kama makubaliano ya biashara huru ilianza kutekelezwa tarehe 30 Mei 2019, lakini biashara yake itaanza rasmi tarehe 1 Juni 2020. Lakini katika hali ya kutatanisha mazungumzo ya kuelewana bado yanaendelea. Wadau wanaohusika bado hawajaafikiana kuhusu aina za ushuru, huduma zitakazotekelezwa, haki za umiliki wa uvumbuzi na mipango ya uwekezaji ambazo zimeratibiwa kumaliziwa mwishoni mwa mwaka 2020.

Kwa hiyo mkataba wa AfCFTA ambao umesainiwa ni muundo tu wa itakavyokuwa, kwani kiini halisi cha makubaliano bado hakijakubaliwa wala kukamilika. Lakini tunajua kuwa matarajio ni makubwa kwa AfCFTA kutoa utaratibu thabiti wa biashara na uhuru wa uwekezaji ndani ya Afrika kupitia njia zinazoonekana katika FTA zingine hadi sasa. Utaratibu utakaoratibiwa utalenga kila uwezo wa taifa husika huku ikiendeleza mtindo thabiti. Umoja wa Ulaya (EU) tayari unazungumza juu ya kujadiliana na maeneo ya kikanda moja baada ya jingine mara baada ya AfCFTA kukamilika.

Kilimo na uzalishaji wa chakula - huchangia asilimia 55 ya nguvu kazi barani Afrika na ndio mwajiri mkubwa wa wanawake – na kwa sasa sekta hiyo ipo chini ya rada ya AfCFTA. Ukubwa huu ndio sababu ambayo AfCFTA inataka kufungua mipaka ya eneo hilo. Hii itasababisha kusambaa kwa bidhaa nje ya ushuru ambao bado haujakubaliwa. Pia inatarajiwa itawezesha wafanyakazi kuwa na uhuru wa kutafuta ajira lakini taratibu za hapo awali kwenye mkataba wa soko la pamoja katika Afrika Mashariki unadokeza kwamba ni watalaamu walio na uzoefu mkubwa tu ndio watanufaika, na si kundi kubwa la ambalo ni la wanawake. La kuhuzunisha ni kwamba mkataba huu utaunganisha mipango ya umiliki na uvumbuzi, pengine kupitia mpango wa umiliki wa mbegu wa UPOV.

Katika sehemu kubwa ya afrika, sio tu kwamba wanawakwe ndio wengi kwenye sekta isio rasmi ya biashara kati ya mataifa mipakani, bali pia biashara zao zimejikita zaidi kwenye nguo, bidhaa za kilimo na bidhaa za

matumizi za nyumbani ambazo huzifanya wao binafsi kwa kujitegemea kila wiki. Wanajishughulisha na idadi ndogo ya bidhaa ambazo huwafanya kuvuka mipaka mara kwa mara na hivyo kufanya shughuli zao kuwa aghali sana. Kwa kawaida hukumbana na unyanyasaji wa kijinsia, ukosefu wa maarifa juu ya kanuni na taratibu za biashara, ufahamu duni kuhusu masoko, na kukumbana na hali hatarishi ya kimwili. Mkataba wa AfCFTA, wenye azimio kuu la kuimarisha biashara huru na makampuni tajiri hautafanya chochote kuwasaidia wanawake hawa.

Sehemu nyingine ya AfCFTA iliyo na athari kubwa kwa wanawake ni Mipangilio Maalum ya Uchumi *(Kwa Kiingereza: Special Economic Arrangements)*. Kama inavyotarajiwa pendekezo hili ni kuwezesha taifa husika kuvutia na kukuza wawekezaji wake wa ndani kupitia maeneo kamili ya biashara na viwanda kwa lengo la kuleta "maendeleo". Lakini jinsi hili litakavyotekelezwa ni la kusubiriwa, lakini kutokana na uzoefu wa mipango kama hiyo sehemu mbalimbali duniani, kwa hakika ni lazima mipango hiyo itakuwa na madhara kwa wanawake.

Hitimisho

Tukiangalia historia ya mikataba ya kibiashara barani Afrika, na mapambano dhidi ya mikataba hiyo kwa miaka 30 iliyopita, mtu anapaswa kujiuliza: Je, mikataba hiyo imeimarisha jukumu la wanawake katika jamii? Je, mikataba hiyo imewainua wanawake kiuchumi, kijamii, kitamaduni, na kisiasa? Je, mikataba hii inatoa nafasi ya kazi nzuri ambazo husaidia wanawake kukidhi mahitaji ya familia zao, kufurahia afya kamili na haki za uzazi? Pia kwa mapana zaidi, Je, wanaunga mkono au badala yake wanakandamiza masoko yasiyo rasmi ambayo ni aslimia 60% ya ujenzi wa uchumi barani Afrika?

Kwa hakika mikataba yote ya biashara imeshindwa kujibu maswala haya yote. Vitendo vinazungumza zaidi kuliko maneno, na ni wazi kuwa matokeo ya FTAs kwa watu wa chini yanasaliti huduma-ya-mdomo toka kwa wafadhili kwenda kwa wanawake na sekta nyingine zilizo pembezoni. Msingi wa nadharia mamboleo na huria wa tawala hizi za biashara uko kila mahali na kwa vitendo ni mashine inayoendeshwa na sekta ya makampuni. Tunahitaji mbinu mpya ya biashara, mikakati mipya inayotegemea maadili tofauti kabisa: mikakati ambayo ni endelevu, ya pamoja, isiyo na ukoloni na isiyo na mfumo-dume, mikakati inayotambua na kushughulikia mahitaji na matakwa ya watu wa Kiafrika.

PICHA ZILIZO NA MAELEZO ZAIDI:

COVID-19 imetoa mwanya kwa serikali kusini mwa jangwa la Sahara barani Afrika kupata kisingizio cha kukandamiza wauzaji wasio rasmi, bila kujali kuwa wanawake wanaofanyakazi katika sekta hii isiyo rasmi wanatoa huduma muhimu kwa familia zao na jamii.

Polisi wa Uganda, Kitengo cha Ulinzi wa Mitaa (LDU) Na jeshi huko Kampala wakitekeleza agizo la rais kupiga marufuku ushafirishaji wa umma na masoko yote yasiyokubali ya chakula kama njia ya kudhibiti kuenea kwa virusi vya Korona. Mpiga picha: Kampala dispatch.

Wauzaji wa matunda wanafukuzwa kutoka mitaa ya Kampala, Uganda. Mpiga picha: Badru Katumba/AFP kupitia Picha za Getty.

Notes

1. Kennedy Senelwa, "East Africa exports to the US hit $1bn in the year to September 2018", The East African, 31 December 2018, https://www.theeastafrican.co.ke/business/East-Africa-exports-to-the-US-hit--1bn-in-the-year-to-September/2560-4914404-12mqfte/index.html
2. Timothy Kalyegira, "What failure of AGOA says about Africans", Daily Monitor, 24 May 2015, https://www.monitor.co.ug/OpEd/Commentary/failure-AGOA-Africans/689364-2727256-i5vcix/index.html
3. UNCTAD, June 2019: https://unctad.org/en/pages/PressRelease.aspx?OriginalVersionID=520
4. Joachim Jarrreau, et al. "Lifting the lid on the black box of informal trade in Africa," The Conversation, September 2018: https://theconversation.com/lifting-the-lid-on-the-black-box-of-informal-trade-in-africa-102867
5. "Informal trade may hold the key to food security", Fin24, 20 Oct 2018, https://www.fin24.com/Opinion/informal-trade-may-hold-the-key-to-food-security-20181017
6. GRAIN and AFSA, "The real seed producers", 2018, https://grain.org/e/6035
7. A good summary from Latin America is provided by Graciela Rodríguez, "Impacts du libre-échange sur les femmes dans un monde globalisé", in Alternatives sud, vol. 24, 2017, pp. 147-165. From Asia, please see the excellent materials from Asia-Pacific Forum on Women, Law and Development at https://apwld.org/tag/trade-liberalization/
8. See bilaterals.org website for many accounts, and particularly bilaterals.org, BIOTHAI and GRAIN, "Fighting FTAs", 2008, https://www.bilaterals.org/fightingFTA-en-Hi.pdf
9. See GRAIN, "Trade agreements privatising biodiversity outside the WTO: 2018 update", https://grain.org/e/6030. UPOV is a French acronym for Union for the Protection of New Plant Varieties, a type of patent regime for seeds.
10. See GRAIN and AFSA, "Th real seed producers", 2019, https://grain.org/e/6035
11. AFTINET, "293 community Groups Call on World Trade Organization to stop other negotiations and focus on access to life-saving medical supplies", 20 April 2020, http://aftinet.org.au/cms/node/1859
12. See for example Eric Toussaint et al., "South Africa's Special Economic Zones in Global Context," ACCEDE, September 2019: https://accede.co.za/wp-content/uploads/2019/09/ACCEDE%20&%20FES%20Policy%20Working%20Paper%20No.1_WEB.pdf
13. See GRAIN, "Supermarkets out of Africa! Food systems across the continent are doing just fine without them", November 2018, https://grain.org/e/6042
14. See RADD, Muyissi Environnment, Culture Radio, Natural Resource Women Platform, GRAIN and WRM "Breaking the silence: Industrial oil palm and rubber plantations bring harassment, sexual violence and abuse against women," March 2019: https://grain.org/e/6164
15. "Tanzania's horticulture industry gets new lease of life", The Citizen, 14 April 2020, https://www.thecitizen.co.tz/news/business/Horticulture-gets-new-lease-of-life/1840434-5523522-exursez/index.html
16. Claire Felter, "What would a US-Kenya trade deal mean?", Council on Foreign Relations, 21 Feb 2020, https://www.cfr.org/in-brief/what-would-us-kenya-trade-deal-mean. From 2002-2017, US counterterrorism assistance spending in Africa was highest in Kenya ($9.2bn). See Stimson Study Group on Counterterrorism Spending, May 2018, https://www.stimson.org/wp-content/files/file-attachments/CT_Spending_Report_0.pdf
17. SEATINI Uganda, "Free movement of workers in the East African Community: Implications for youth employment in Uganda", 2014, https://www.seatiniuganda.org/publications/research/35-free-movement-of-workers/file.html
18. EASSI, "Women informal cross border traders: Opportunities and challenges in the East African Community", 2012, https://eassi.org/wp-content/uploads/2019/07/Women-Informal-Cross-Border-Traders-Opportunities-and-Challenges-in-the-EAC-Action-research-2012.pdf
19. United Nations Conference on Trade and Development, "Borderline: Women in informal cross-border trade in Malawi, the United Republic of Tanzania and Zambia", 2019, https://unctad.org/en/PublicationsLibrary/ditc2018d3_en.pdf

Kiambatanisho 1: Masharti ya Kustahiki ya AGOA

(a) KWA UJUMLA.— Raisi amepewa mamlaka ya kuteua nchi ya Kusini mwa Jangwa la Sahara kuwa nchi inayostahiki katika nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Kusini mwa Sahara hasa ikiwa Raisi atajiridhisha kuwa nchi hiyo:

(1) imeanzisha, au ikiwa inafanya maendeleo endelevu kuelekea kuanzisha—

(A) uchumi unaotegemea soko ambao unalinda haki na mali za watu binafsi, unaojumuisha mfumo wa wazi wa kibiashara kwa mujibu wa sheria, na unaopunguza uingiliaji wa serikali katika uchumi kupitia hatua kama udhibiti wa bei, ruzuku, na umiliki wa serikali wa mali za kiuchumi;

(B) utawala wa sheria, vyama vingi vya kisiasa, na haki ya mchakato unaostahili, kesi zinazozingatia haki, na ulinzi sawa chini ya sheria;

(C) kuondoa vizuizi kwa biashara na uwekezaji wa Marekani ikiwa ni pamoja na—

(i) utoaji na uwepo wa utendaji wa kitaifa na hatua za kutengeneza mazingira yanayofaa kwa uwekezaji wa ndani na ule wa nje;
(ii) ulinzi wa miliki; na
(iii) utatuzi wa migogoro ya kibiashara na uwekezaji baina ya nchi mbili;

(D) sera za kiuchumi zinazolenga kupunguza umaskini, zinazo ongeza upatikanaji wa huduma za afya na fursa za elimu, zinazopanua miundombinu, zinazo hamasisha uendelezaji na ukuzaji wa biashara binafsi, na zinazounga mkono uundaji wa masoko ya mitaji kupitia mikopo midogo midogo au kupitia programu zingine;

(E) mfumo wa kupambana na ufisadi na rushwa, kama vile kusaini na kutekeleza Mkataba wa Kupambana na Rushwa kwa Maafisa wa Kigeni wa Umma katika shughuli za Biashara za Kimataifa; na

(F) ulinzi wa haki za wafanyakazi zinazotambulika kimataifa, ikiwemo haki za ushirikiano, haki za kuandaa na kujadiliana kwa pamoja, marufuku ya matumizi ya aina yoyote ile ya kazi ya kushurutishwa au ya kulazimishwa, umri wa chini wa kuajiriwa kwa watoto, na hali zinazokubalika za kufanya kazi kwa kuzingatia kiwango cha chini cha mshahara, masaa ya kazi, na usalama kazini na afya;

(2) haishiriki katika shughuli zinazo dhoofisha usalama wa kitaifa wa Marekani au maslahi ya sera za nje za Marekani; na

(3) haishiriki katika ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu zinazotambuliwa kimataifa au haiungi mkono vitendo vya ugaidi wa kimataifa na baina ya mataifa na iwe inashirikiana katika juhudi za kimataifa za kukomesha ukiukwaji wa haki za binadamu na shughuli za kigaidi.

(b) MWENDELEZO WA UTII.—Ikiwa Raisi ataamua kwamba nchi mojawapo iliyopo kusini mwa Jangwa la Sahara haifanyi maendeleo ya kukidhi mahitaji kama yalivyoelezwa katika kifungu kidogo cha (a) (1), Raisi atasitisha uteuzi wa nchi hiyo kulingana na kifungu kidogo cha (a).

GRAIN

THE SUHODE FOUNDATION
THE SUHODE FOUNDATION

Seed Savers Network
Kenya